

**MAELEZO KWA WAOMBAJI WA ULINZI WA KIMATAIFA (HALI YA UKIMBIZI NA HIFADHI MBADALA)**

**KUANZISHWA KWA SHERIA YA ULINZI WA KIMATAIFA YA 2015**

Mwombaji Mpendwa:

Ninarejelea maombi yako ya sasa ya hali ya ukimbizi/hifadhi mbadala.

Ninakufahamisha kuwa mipango mipya ya uchunguzi na ubainishaji wa maombi ya ulinzi wa kimataifa (hali ya ukimbizi na hifadhi mbadala) na kibali cha kusalia Nchini itaanzishwa katika Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015 (Sheria ya 2015) ambayo inastahili kuanzishwa na Tánaiste na Waziri wa Haki na Usawa **mnamo tarehe 31 Desemba 2016.**

Chini ya Sheria ya 2015, Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi (ORAC) inaondolewa na jukumu la uchunguzi wa maombi ya ulinzi wa kimataifa litahamishwa kwa Ofisi mpya ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO) katika Huduma ya Uandikishaji na Uhamiaji ya Ayalandi. Mahakama ya Rufaa ya Wakimbizi (RAT) inabadilishwa na Mahakama ya Rufaa la Ulinzi wa Kimataifa.

Sheria ya 2015 ina matoleo ya mpito yanayohusiana na (i) maombi ya hali ya ukimbizi na hifadhi mbadala yaliyowasilishwa kwa ORAC na (ii) maombi ya rufaa yaliyowasilishwa kwa RAT kabla ya kuanzishwa kwa Sheria ya 2015.

**Kulingana na mahitaji ya matoleo ya mpito katika Sheria ya 2015, tutawasiliana na wewe Januari 2017 kama taratibu hizi mpya katika Sheria ya 2015 zitatumika kwenye maombi au rufaa yako iliyopo. Unaweza pia kuombwa wakati huo utoe maelezo ya ziada ya kusaidia katika kuchakata maombi yako. Tafadhali kumbuka kwamba hauhitaji kuchukua hatua yoyote hadi usikie kutoka kwetu.**

Iwapo utabadilisha anwani yako kwa sasa tafadhali tueleze kwa kuwasiliana na Customer Service Centre, ORAC/IPO, 79/83 Lower Mount Street, Dublin 2.

Maelezo haya yanakiliwa kwa wakilishi wa kisheria.

**Huduma ya Uandikishaji na Uhamiaji ya Ayalandi,  
Desemba 2016**

NAKALA YA MAELEZO HAYA, AMBAYO HAIONYESHI KUTOA UWAKILISHI WA KISHERIA WA SHERIA YA ULINZI WA KIMATAIFA, 2015, INAPATIKANA KWA LUGHA MBALIMBALI KWENYE TOVUTI YA ORAC ([www.orac.ie](http://www.orac.ie)) CHINI YA OFISI YA ULINZI WA KIMATAIFA.

Swahili